Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 12 Oktoba, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

TAARIFA YA NAIBU SPIKA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi cha tarehe 5/10/2017 na tarehe 6/10/2007, Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma, Nafasi za Wanawake na Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa waliuliza maswala ya nyongeza kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto na Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto, aliahidi kujibu kwa maandishi. Sasa namuomba Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto asome majibu ya maswala ya nyongeza yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe hao.

Waheshimiwa Wajumbe, aidha, katika Kikao cha tarehe 4/10/2017, Mhe. Panya Ali Abdalla aliuliza swali la nyongeza kwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na Mhe. Naibu wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira aliahidi kujibu kwa maandishi, Waheshimiwa Wajumbe. Sasa namuomba Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira asome jibu la swali la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Mjumbe huyo.

Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa heshma na taadhima kwanza napenda ifahamike kuwa wizara yangu kupitia Kamisheni ya Kazi haisajili Vikundi vya Uwakala isipokuwa inatoa leseni ya Uwakala Binafsi kwa ajira kwa taasisi, ambazo zimetimiza vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Ajira Nam. 11 ya 2015. Ambapo Sheria hiyo imempa Mamlaka kamili Kamisheni wa Kazi kutoa leseni hiyo.

Hadi sasa ni taasisi kumi na mbili, za Uwakala Binafsi wa ajira ndizo ambazo zina leseni hai na zinahusika na kuwapatia vijana wetu kazi nje na ndani ya nchi. Taasisi hizo ni kama ifuatavyo:

1. *Blue Agency*
2. *Global Manpower Partners Agency*
3. *Sugetra Tour and Recruitment Agency Limited*
4. *Khafamo's Group Company Limited*
5. *Suhail Company Limited*

6. *Tamha Agency & Global Employment*
7. *Rays Development Company Limited*
8. *Talent Man Power Agency*
9. *Empowerment of Youth Agency Limited*
10. *Mwasum Star Commission Agent Corporation Limited*
11. *Three Brothers Agency Limited*
12. *Global Job –Links Agent Company Limited*

Aidha Mhe. Naibu Spika, wakati najibu swali la Nam. 95 niliulizwa swali la nyongeza kwa Mhe. Salha Mahamed Mwinjuma, aliyetaka kujua ni vijana wangapi walikwenda nje ya nchi. Kuanzia 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, jibu la suala hili ni kama ifuatavyo:

Kupitia Kituo chetu cha Taarifa za Soko la Ajiri, taarifa zinaonesha kuwa kuanzia Julai, 2016 mpaka Julai 2017, vijana elfu moja na thalathini na nane (1,038) Wanaume 328, na Wanawake 710 wamepata fursa za Ajira nje ya nchi ambapo Abudhabi wamekwenda Vijana 7 (Wanaume 5, Wanawake 2) Djibouti Vijana 8 (Wanaume 6, Wanawake 2) Oman Vijana 815 (Wanauume 141, Wanawake 674). Qatar Vijana 81 (Wanaume 74, Wanawake7) Saudi Arabia Vijana 11 wote ni Wanaume na U.A.E wamekwenda Vijana 116 (Wanaume 91, Wanawake 25).

Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto. Sasa nimpe nafasi Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati, na Mazingira ambaye atajibu swali la Mhe. Panya Ali Abdalla. Karibu Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, Wakati ninajibu swali Nam. 6, niliulizwa swali la nyongeza na Mhe. Panya Ali Abdalla aliyetaka kujua idadi ya fedha zinazohitajika kwa ajili ya kukamilisha mradi wa ujenzi wa *tank* la maji na kisima kilichopo Mchekeni Upenja, Jimbo la Kiwekwa.

Mhe. Naibu Spika, jibu la swali hilo ni kama, fedha zinazohitajika ili kukamilisha mradi huo ni shilingi 608,872,260/-. Ahsante sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais): Mhe. Naibu Spika, naomba kuweka Mezani Mswada wa Kufuta Sheria ya Uchaguzi, Sheria Nam. 11 ya mwaka 1984 na kutunga Sheria ya Uchaguzi ya 2017, na maswala mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Mezani Mswada wa Sheria ya

Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, na kuweka vifungu vya usajili na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. (Kny. Mhe. Waziri wa Biashara na Masoko): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda, nipo hapo kujibu maswali ya …

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, sio kujibu maswali ni Hati za kuwasilisha Mezani, Mhe. Waziri naomba mmsaidie Waziri kumpa hiyo *order paper*. Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi . *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi (Kny. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko): Naomba kuweza kuweka Mezani, Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati Zanziabr pamoja na kuwawezesha Ushajiishaji na Uendelezaji waViwanda Vidogo Vidogo na vya Kati, Zanzibar na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa, Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Naibu Spika, Naomba kuweka Mezani Hati ya Mswada wa Marekebisho ya Sheria mbali mbali na kuweka Masharti bora ndani yake na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Naibu Spika. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katibu.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 111

Wanafunzi Kuchukia Somo la Sayansi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali alitamka wakati wa kukabidhi mashine ya fotokopi Skuli ya Donge, kuwa wanafunzi hawapendi kusoma masomo ya sayansi na ndio sababu Zanzibar ikawa na upungufu mkubwa wa walimu ya sayansi.

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara yake haioni kuwa kwa kauli hii aliyoitoa inazidi kuwavunja moyo hao wanafunzi wachache ambao wangependa kusoma sayansi,

(b) Je, Mhe. Wizara haioni kuwa kutofanywa vizuri somo hilo wanafunzi wanapofanya mitihani ndio sababu wanafunzi wengi wanachukia somo hilo.

(c) Je, wizara haioni kuwa kutotayarishwa vizuri kwa wanafunzi ndio sababu wanafunzi kutolifanya vizuri somo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, swali lake Nam. 111 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Kauli niliyoitoa ya wanafunzi kutopenda masomo ya sayansi ndio sababu ikawa na upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi haikuwa na lengo la kuwavunja moyo, bali ninaamini kauli ile itawashajihisha kuongeza bidii katika kuyapenda na kuyasoma masomo hayo, ili wapate fursa nzuri katika soko la ajira na kupunguza tatizo la uhaba wa walimu wa sayansi na wataalamu wengine.

Mhe. Naibu Spika, wanafunzi hawachukii masomo ya sayansi kwa sababu ya kutofanywa vizuri masomo hayo, bali kutofanya vizuri mitihani yao inatokana na upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi, vifaa vya maabara vya kusoma kwa vitendo, vifaa vya kufundishia na kujifunzia wanapokuwa katika masomo hayo.

Hata hivyo, wizara yangu inafanya kila jitihada ya kuhakikisha wanafunzi wanapenda masomo ya sayansi na wanafaulu vizuri katika mitihani yao. Miongoni mwa juhudi hizo ni pamoja na kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia *SUZA* katika kuandaa programu ya mafunzo ya sayansi kwa walimu wasiopungua 600 wa sanaa ambao kwa sasa wanafundisha masomo ya sayansi kwa walimu wasiopungua mia 600 wa sanaa ambao kwa sasa wanafundisha masomo sayansi katika skuli zetu za serikali. Pia, kujenga maabara katika skuli 25 zikiwemo 15 Unguja na 10 Pemba, kuzipatia fedha za ruzuku skuli za sekondari za serikali kwa lengo la kuwajengea uwezo walimu na uongozi wa skuli kununua na kufanya maamuzi sahihi. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kwanza usikatae. Mhe. Naibu Waziri kauli uliyotoa ilikuwa inawavunja sana wanafunzi na hiyo imeripotiwa katika vyombo vya habari hata katika mitandao ya jamii imeripotiwa hicho kitu.

Kwanza inavyoonekana serikali haijafanya tathmini ya kubaini tatizo la wanafunzi kutopenda masomo ya sayansi na jambo ambalo tumelishuhudia, Zanzibar ufaulu wake katika masomo ya sayansi limekuwa dogo chini swali.

(a) Je, serikali au wizara ina mpango gani wa muda mrefu wa kuandaa walimu wa sayansi wa kutosha, ili kukidhi mahitaji ya walimu wa sayansi.

(b) Tumeshuhudia Tanzania Bara ujenzi wa maskuli, kuna agizo ikajengwa skuli ijengwe na maabara pale pale. Katika jibu lake kuna skuli kama 25 wamejipangaje wanapojenga skuli na maabara iwepo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imejiandaa vya kutosha, ili kuona katika kipindi kifupi kinachokuja inajitosheleza kwa walimu wake wa sayansi. Imejiandaa kwanza kwa kuwa katika vyuo vya ndani ya Zanzibar kuanzisha masomo ya sayansi kwa vijana wetu katika ngazi ya Diploma, Ngazi ya Shahada ya kwanza na hata Ngazi ya Shahada ya Pili, zinatolewa hapa hapa Zanzibar kupitia Chuo Kikuu cha *SUZA*.

(a) Kuna mafunzo ambayo kwa sasa yana wanafunzi wengi ambao wanasoma sayansi, kwa hivyo tunatarajia katika kipindi kifupi sana Zanzibar itaweza kulitatua tatizo hili la upungufu wa walimu wa sayansi hata hivyo, kwa hawa walimu walioko ambao tulisema kwamba walikuwa awali katika muelekeo wa kusomesha masomo ya sanaa, wamepewa mafunzo ya kutosha na wataendelea kupewa mafunzo ya kutosha ya ndani ya nchi na nje ya nchi ili kuona wanamudu vyema. Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa kuna baadhi ya walimu hawa, ambao tunasema kwamba wanashahada za sanaa, lakini wanasomesha sayansi, baada ya mafunzo haya kulingana na ukaguzi tunaofanya wanaendelea kufanya wanaendelea kufanya vizuri zaidi.

(c) Tunaposema skuli 15 Unguja 10 Pemba hizi ni katika muelekeo wa sasa wa kufufua sayansi masomo ya sayansi lakini kwa kweli kila skuli inatarajiwa na hakika ndivyo ilivyo ina maabara yake. Kwa hivyo tunaposema ni miradi mipya ya kuimarisha lakini kila skuli ina maabara zake na zinasomesha masomo haya ya sayansi tatizo kama tunavyosema ni upungufu. Lakini nimuhakikishie kwamba kwa upande wa walimu wa sayansi wa *Biology* na *Chemistry* hawa tunao, tatizo ni katika *Mathematics* na *Physics* na haya tunafanya kazi. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana, Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kwa kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya kusikitisha ya Mhe. Naibu Waziri kwa sababu kwanza kumuona Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa taarifa yako kama tuliokuweko kwenye kijiwe.

Mhe. Naibu Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba katika muda mfupi walimu hawa watapatikana, na humu tukaona kwamba wanafunzi wanapata tabu na wanateseka je, ni lini mwakani, keshokutwa hiyo kama alivyosema yeye au lini tunataka kujua ule muda lini. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Suleiman Makame Ali, swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Serikali inapotoa majibu yake inatoa kwa uhakika, kwa utafiti kabisa haibahatishi lakini kwa bahati mbaya inawezekana baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi wahawaelewi yale masuala yenyewe na ndio maana wakawa wanadhihaki jambo. Sisi tunazo taarifa za kutosha juu ya tunayojibu, yaani tunazo taarifa za kitakwimu pamoja na za hali halisi.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba suala la ajira la watu wa sayansi na ajira nyengine ni mchakatu, ni suala linaloendelea na ndio maana si kwamba tunasubiri tushitosheleze, ili

masomo hayo yasomeshwa. Hivi sasa hakuna somo hata moja ambalo halisomeshi la sayansi na tukasema kwamba tunakwenda hatua kwa hatua tulikuwa tunaagiza wenzetu kutusaidia katika masomo ya *Biology* na *Chemistry* hayo sasa hatuagizi tena, tumebakia katika masomo ya *Mathematics* na *Physics.*

Kwa hivyo tunapotowa jawabu tunatoa kwa uhakika. Ahsante.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu Uratibu Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Kuhusu utaratibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Kanuni ya 63(37) alichouliza Mhe. Suleiman Makame Ali amezoea majibu alisema Naibu Waziri alipojibu. Muda mfupi tu watapatikana walimu wa sayansi, sasa alichozungumza Mhe. Suleiman Makame ni lini mwezi ujao, mwakani, kesho kutwa ili wananchi wangu wa Mkia ng'ombe na Paje, ili wapate walimu wa sayansi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika bado tunasema kwamba huu ni mchakato na hivi sasa tuko katika hatua za mwisho za ajira ya walimu wakiwemo walimu wa sayansi kama mia 200. Utaratibu huo uko hatua za kiutumishi, usaili umeshafanyika uteuzi utafanyika. Uteuzi mara baada ya kufanyika na kukamilika walimu hawa watasambazwa katika skuli zinazohusika.

Nam. 2

Agizo la Serikali Kuhusu Kuhama Watu Wanaoishi Mabondeni

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: (Kny: Mhe. Abdalla Maulid Diwani) – Aliuliza:-

Serikali imewataka watu wote wanaoishi mabondeni kuhama pamoja na kuvunja makaazi yao.

(a) Je, serikali kupitia wizara yako imechukua jitihada gani katika kuwapatia viwanja au makaazi bora watu wa mabondeni.

(b) Ni lini wizara yake itawaondoa watu hawa sehemu hatarishi kwa njia sahihi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake Nam. 2 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, serikali imekuwa ikihamasisha wananchi wasijenge katika maeneo ya mabondeni ambayo ni hatarishi kwa maisha na afya za wananchi. Hata hivyo, serikali kupitia Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi ya Miji *(Master Plan)* imeainisha maeneo ambayo yanapaswa kuendelezwa kwa makaazi.

Hivyo, kupitia Mpango huo, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kushirikiana na wadau, wafadhili na wananchi, imeainisha maeneo ya makaazi kwa ujenzi wa nyumba katika maeneo tofauti.

(b) Mhe. Naibu Spika, kama ilivyoelewekwa kwamba suala la maafa linaratibiwa na Kamisheni ya Maafa iliomo ndani ya Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Lakini wizara yangu kwa kushirikiana na Kamisheni ya Maafa na Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ zinaendelea na utaratibu utakaowawezesha wananchi kuondoka katika maeneo hatarishi. Ahsante.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake haya ya ufasaha, lakini naomba kumuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa mpango huu ni wamuda mrefu na pia ukizingatia wananchi wetu bado wanahitaji nyumba za kuishi. Je, Mhe. Naibu Waziri ni lini hasa ujenzi huwo utaanza kujengwa ili wananchi wetu wafaidike na matunda haya ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza napokea pongezi hizo. Lakini pili naomba nimwambie kwamba huu utaratibu ambao unaratibiwa kama nilivyokuwa nimesema siyo la Wizara ya Ardhi peke yake ni la mtambuka. Sasa baada ya utaratibu kukamilika kwa sababu tumejifunza kitu huko nyuma tunaondosha lakini baadaye athari inarudia tena. Lakini baada ya utaratibu huu kukamilika na kuhakikisha kwamba kinachofanyikana hakuna tena mwanya wa kurudi tena wananchi katika maeneo hatarishi itafanyika. Ahtente sana.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Naibu Spika, swali langu la nyongeza. Je, wakati huo watu wanajenga kwenye mabonde au kwenye sehemu hatarishi, serikali inakuwa iko wapi. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu juzi hapa nimeuliza kuna maeneo yamejengwa na kuna mabomba ya maji yapo barabarani sikupata jibu. Sisemi kwamba serikali inashiriki moja kwa moja lakini inashiriki. Mwanakwerekwe maji yanaziba tunatoa vibali, juzi tumetoa vibali kutoka Mwanakwerekwe kwenye *junction* kwenda Amani, maduka yapo barabarani chini kuna paipu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa uliza swali.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Swali langu serikali inafanya nini, hatuwezi kusema kwamba labda serikali ipewe adhabu ama nini. Lakini Mhe. Naibu Spika, serikali ilikuwepo wapi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Serikali ipo kila siku lakini na hawa niseme wananchi wanajaribu kutumia akili za ziada katika kufanya jambo ambalo wanataka kulifanya. Ni sawa kama vile wewe una nyumba yako una geti,

una mlinzi lakini pengine inatokezea bahati mbaya unaibiwa. Siyo kama umejisahau bali ni kutokana na hali yenyewe.

Lakini pia nimegunduwa kuna watu wanasubiri siku ya Jumamosi ama Jumapili kwa kuona kwamba serikali kama ulivyokuwa umeuliza labda hawapo kazini. Lakini tumegundua na tutalisimamia katika kuliweka sawa. Lakini kwa indhari hiyo hiyo ambayo unayoisema kwa muono huo huo ambao umeuona ndiyo maana tukasema kwamba baada ya utaratibu ambao tumeupanga na ukapangika tutaweza kudhibiti yote haya ambayo umeyasema Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Waziri wakati anajibu masuala yake amesema kwamba wananchi wanafanya hadaa ya kujenga siku ya Jumamosi na Jumapili ambapo ni siku za mapumziko. Je, kwa nini wanapoamka siku ya Jumatatu serikali isivunje.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kwamba siyo busara sana kwamba kila wakati uvunje. Mara nyingi tunakwenda na utaratibu kwa sababu hawa wote ni wananchi wetu na tunataka wananchi wetu wapate makaazi bora, lakini pia wawe salama. Sasa siyo kufukuzia katika kuvunja bali katika kuwaelekeza wapi wanastahiki kujenga na itakapotokezea kwamba tumemkuta anajenga katika hatua ya awali tunamzuia. Ndiyo maana kuna chombo kinaitwa *DCU* kazi yake ni hii kuangalia kwamba watu wanajenga kwa kufuata *master plan* ya miji. Ahsante sana.

Nam. 71

Wizara Kushindwa Kudhibiti Ongezeko la Kesi za Udhalilishaji

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Taarifa mbali mbali zimetolewa kuhusu ongezeko la kesi za udhalilishaji kwa mwaka 2017 pamoja na kelele, mipango, mikakati na hatua chungu nzima zilizoahidiwa kuchukuliwa na wizara kukabiliana na vitendo hivyo.

(a) Je, kwanini wizara haisemi kama imeshindwa katika mapambano dhidi ya vitendo vya udhalilishaji.

(b) Je, kuna mikakati gani zaidi wizara inakusudia kufanya zaidi ya hiyo iliyokwishaelezwa kabla ya kukabiliana na ongezeko la vitendo hivyo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 71 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kwanza sikubaliani na swali lililoulizwa la Mhe. Mwakilishi kwamba wizara imeshindwa katika mapambano dhidi ya vitendo vya udhalilishaji. Wizara kwa

kushirikiana na wadau mbali mbali imefanya juhudi za kusimamia mapambano hayo kupitia Kampeni ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein 'Maliza Udhalilishaji', Kamati ya Kitaifa ya Kupambana na Vitendo vya Udhalilishaji na Wanawake na Watoto na Operesheni Maalum ya Maliza Udhalilishaji. Pia, kwa kushirikiana na Mashirika ya Kimataifa kama vile *Save the Children, UNICEF, UN Women na UNFPA*, Wizara imesimamia uratibu wa mapambano hayo. Matokeo yake uelewa wa jamii umeongezeka na kiwango cha kuripoti matokeo hayo kimeongezeka sana.

(b) Mhe. Naibu Spika, Mkakati uliopo ni Mpango wa miaka mitano wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto (2017–2022). Mkakati huu umejikita kwa namna ya kipekee kuyashughulikia masuala haya hasa kwa kutilia mkazo suala la kukinga vitendo hivi visitokee na kuweka mikakati ya kuinarisha utoaji wa huduma pale yanapotokea. Pia, mpango huu umeipa nafasi kubwa familia katika masuala ya ulinzi wa watoto pamoja na kuhimiza mila na desturi ambazo zinazuia na kudhibiti vitendo vya udhalilishaji na ukatili nchini.

Mhe. Naibu Spika, kwa kupitia kiti chako, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kuunga mkono utekelezaji wa mpango huo katika majimbo yao na kwa nafasi zao. Tushirikiane katika kulisimamia suala hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri hakubaliani na Mwakilishi jibu hilo sasa hivi itabidi akubali. Majibu haya tumekuwa tukiyazoweya siku zote alisema kuna mikakati ya miaka mitano, kuna timu ya kitaifa lakini bado ndiyo kwanza vitendo vya kudhalilisha watoto vinazidi siku zote na vyombo vya habari vinaripoti.

a) Kwa nini hasemi sasa hivi kwamba Wizara imeshindwa kulisimamia tukio hilo, hilo mwanzo.

b) Mila na desturi za kudhibiti vitendo vya udhalilishaji inaonekana kuna desturi mbovu na mbaya zinaingia katika mila zetu, kwa mfano kukithiri kwa mabaa, kumbi za starehe. Je, serikali iko tayari sasa kuzuia kutokujengwa kwa mabaa na kumbi za starehe, ili vitendo vya maadili visiporomoke.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

a) Kama yeye ni Mwakilishi anisaidie kwa nini vitendo vinazidi wakati tunapiga kelele na suala hili nadhani ni *attitude* iko ndani ya vichwa vya watu. Hivyo, yeye kama ni Mwakilishi najua anaweza kutusaidia sana kwa kuanza na wengine wote Wawakilishi wenzangu kwa kuanza kufanya kazi hizi na kuhakikisha kwamba wale wote ambao wanafanya vitendo vya ukatili wanajulikana katika maeneo yao, tukishirikiana itakuwa haviwezi kuongezeka.

Wizara yetu ni kushajihisha mpaka pale wananchi wenyewe watakapoamua na kutambua kwamba suala hili si zuri litatokomea. Hii ni *attitude* ambayo imekuwa kama vile tulivyoanza na Ukimwi tulianza kukemea muda mrefu lakini mpaka leo UKIMWI ni zaidi ya miaka ishirini na ngapi bado unaendelea na suala linaendelea. Naomba tushirikiane na wala tusikate tamaa na wala lisitupiwa kwa wizara pekee yake ni letu sote tushirikiane, tupange mikakati ya hali na mali.

b) Mhe. Mwenyekiti, masuala haya yanaondokea katika sehemu mbali mbali ambazo zinafanywa katika kumbi mbali mbali za starehe ni bahati mbaya sana wanapokuja kuomba vibali hawaelezi wanakwenda kufanya shughuli gani, wengi wanakuja kwa ajili ya *birthday*, wengine wanakuja kwa ajili ya harusi, matuko yanayotokea hukondani ndiyo yanayokuwa na matatizo. Kwa hivyo, hayo pia sisi tumeanza kuyafatilia na kuhakikishwa kwamba pale pale tutakapokuwa tumefanya katika kumbi zetu za serikali kuhakikisha kwamba zinafuatiliwa.

   Nadhani mmeona kabisa juhudi za viongozi Wakuu wa Mikoa wanavyofanya kazi kwa pamoja kwakuhakikisha kwamba kumbi hazitumiki vibaya na vijana hawaachiwi. Lakini pia naomba nitoe wito kwa wazazi, kwani wao ndio wanaoagwa na watoto, wanaonunua mavazi, na wanaotoa pesa wanaowalisha vyakula vizuri wakawa na nguvu za kutosha kwenda kufanya shughuli hizo. Tukishirikiana sisi sote jambo hilo litakwisha. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub basi utaratibu.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu marefu ya Mhe. Waziri ningependa kumuuliza kwamba tunafahamu moja ya mikakati ambayo Kamati ya Kitaifa inachukua kupambana na udhalilishaji ni kuwa na siku maalum ambayo Mahakama zetu huwa zinasikiliza hizi kesi za udhalilishaji. Je, ni kila baada ya muda gani hili hufanyika Mahakama kusikiliza kesi hizi. Tulisikia siku moja tu halafu hatukusikia tena.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, naomba arudie tena alisema ni kitu gani kabla ya kusema ni siku gani maalum. Huku kuna *echo* ni vizuri kusogea akatamkaa vizuri nikasikia vizuri.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Wanu Hafidh Ameir rudia swali.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Moja ya mikakati ya Kamati ya Kitaifa ambayo Mhe. Rais wa Zanzibar ameiyunda ya kupambana na udhalilishaji ni kuwa na siku maalum ambayo Mahakama zetu husikiliza hizi kesi za udhalilishaji. Je, ni kila baada ya muda gani hizi kesi husikilizwa, kwa sababu tulisikia mara moja tu halafu hatukusikia tena kwamba kulikuwa kuna siku maalum kwamba Mahakama zilikuwa zinasikiliza hizi kesi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, itabidi nilifuatilie kwa karibu zaidi lakini ninachojua kwamba kila siku maofisa wetu wanaondoka kwenda kufatilia vituo vyote tunagawana kwenda kuhakikisha kuona kwamba kesi zinafuatiliwa.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza suala dogo la nyongeza.

Tatizo la udhalilishaji linaendelea siku hadi siku na sababu kubwa ya tatizo hili ni kuwa kesi hizi zinatolewa hukumu yake ni muda mdogo. Miaka miwili au miaka mitatu. Je, Mhe. Waziri ni lini serikali italeta Sheria ndani ya Baraza la Wawakilishi ambayo itatoa hukumu ya kifungo cha maisha jela au miaka 30 kama wanavyofanya wenzetu Tanzania Bara. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahante sana Mhe. Naibu Spika, hivi sasa ofisi yangu ya vitengo vya sheria vyote vimekaa kwa ajili ya kupitia kila sheria ambayo tunahisi tunataka kuiboresha ikiwa ni pamoja na hiyo. Lakini hilo pia litategemea nyinyi mtakavyoweza kutuamulia ili tuweze kutoa adhabu ya kiasi gani. Kwa kweli, juhudi ya makusudi vikao tumeshaanza kufanya na sasa hivi tumepeleka taarifa nyingi za kutosha kwa *AG* kwa ajili ya maandalizi ya kuweza kuwasilisha itakapokuwa tayari.

Nam. 133

Umiliki wa Jengo la Kulelea Watoto la Forodhani

Mhe. Suleiman Sarahan Said (Kny Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa) - Aliuliza:

(Mheshimiwa aliyetaka kuuliza swali hilo ameliondowa)

Nam. 26

Kuendelea kwa Vitendo vya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Aliuliza:

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto wa kike na kiume ambapo waathirika wakubwa ni watoto wenye umri chini ya miaka 15, hali inayoashiria janga kubwa katika nchi yetu.

(a) Je, wizara inatoa kauli gani kuhusu tatizo hilo hasa kwa watoto walio chini ya miaka 15.

(b) Je, wizara haioni kwamba wakati umefika kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali waandae Mtaala Maalumu utakaofundishwa kuanzia elimu ya awali (chekechea), ili watoto na vijana wetu wafahamu na kutambua madhara ya jambo hili.

(c) Baadhi ya vijana hao pindi wanapokamatwa na kupelekwa magerezani huendelea na tabia mbaya na hata wanaporejeshwa uraiani. Je, ni hatua gani huchukuliwa na wizara katika kuwarekebisha vijana hao waliokuwa gerezani.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 26 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara yangu inakerwa na kusikitishwa sana na ongezeko la vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa watoto vinavyoendelea kila siku na inasisitiza kuwa suala la kupiga vita vitendo hivi ni la kila mmoja katika jamii ambapo familia ina nafasi kubwa ya kuhakikisha watoto wanalindwa kikamilifu dhidi ya vitendo hivi. Pia, jamii inayowazunguka inatakiwa kuhakikisha mazingira mazuri yanakuwepo kwa watoto kwa ajili ya ustawi wao. Mbali na hayo, taasisi mbali mbali za Serikali na za kiraia ziunganishe nguvu zao kutokomeza matendo haya.

(b) Mhe. Naibu Spika, kuhusu wizara kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuandaa Mtaala Maalum utakaofundishwa kuanzia elimu ya awali. Ushauri umepokelewa na tutaufanyia kazi. Hata hivyo, masuala ya kujikinga na udhalilishaji yanafundishwa katika masomo ya Dini, Sayansi na Sayansi Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeanza kutoa mafunzo hayo katika ngazi ya chekechea.

(c) Mhe. Naibu Spika, watoto wenye umri chini ya miaka 15 hawawekwi magerezani wanapofanya makosa haya isipokuwa wanapelekwa katika Kituo cha Kurekebisha tabia na kupata mafunzo ya kuwa raia wema wa baadae. Kwa wale ambao makosa yao yanalazimisha kupelekwa mahabusu au magerezani. Wizara imefanya juhudi za kuhakikisha kwamba watoto kwenye Magereza hawachanganywi na watu wazima.

Mhe. Sada Ramadhan Mwenda: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri nilikuwa nataka kujua wizara yake inamikakati gani angalau ya kufanya mafunzo hasa tatizo kubwa lipo vijijini la kwenda kuwapa muelekeo angalau wana vijiji kutokana na suala hili. Hujafahamu?

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Bado.

Mhe. Sada Ramadhan Mwenda: Ni hivi, nashukuru sana kwa majibu yako mazuri Mhe. Waziri, swali langu liko hapa la nyongeza. Wizara yake imejipanga vipi kwenda vijijini angalau kwenda kutoa semina kutokana na haya matatizo makubwa yapo vijijini kwa wananchi wetu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, jitihada inafanyika na wizara yangu ambayo kila siku kunatolewa mafunzo mbali mbali kwa njia za semina mbali mbali, kwenye makongamano, katika mashule kwa kutumia *NGO's* mbali mbali na pia vyombo vya habari vyombo ikiwemo televisheni na redio vimekuwa vikitoa taarifa mbali mbali za mafunzo kwa kila siku.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri lakini naomba kuuliza swali dogo.

Je, wizara inampango gani kwa kuanzisha japo vipindi vya redio na televisheni inaanzisha midahalo ambayo wananchi watapata kutoa maoni yao na kwenye makongamano wakatoa maoni yao, kwenye televisheni na midahalo na nyinyi mkapata kuelezea tatizo hili jinsi gani jamii kwa kushirikiana kwa pamoja na wizara inaweza kulimaliza tatizo hili.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu kwamba siyo tunao utaratibu gani, isipokuwa tayari tumeshafanya na ....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, kwa kawaida unapojibu maswali, Mheshimiwa Mjumbe akiuliza swali la nyongeza unanisubiri mimi nikupe ruhusa ya kujibu. Haya Mheshimiwa sasa naomba ujibu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi ni kwamba mpaka sasa hivi hiyo shughuli inafanyika na masomo yanafanyika na mimi mwenyewe nishatoa mafunzo hayo ana kwa ana alfajiri kwenye saa 12:30 mpaka kufika kwenye saa 2:00 au 3:00 kwenye vyomba vya habari mbali mbali ambavyo huwa tunahojiana ana kwa ana. Lakini pia maofisa wangu wamekuwa wakifanya hivyo ni jana tuu wamemaliza vipindi hivyo wakiendelea kutoa maswali na majibu.

Lakini pia hamyapati ipasavyo basi kabla hamjayaeleza tutabidi tutangaze kabla ili watu wajiandae kukaa karibu, ili waweze kuuliza kwa wakati inawezekana wanakuwa hawana taarifa kama tunatoa taarifa hizi.

Mhe. Ali Suleima Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze kwa dhati Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa juhudi mbali mbali ambazo kwenye makongamano na mambo mengine juu ya harakati za udhalilishaji wa watoto wetu katika nchi yetu.

Lakini katika swali langu nataka kumuuliza hivi Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ni muhimu sana kwake yeye katika matokeo mbali mbali yanayotokea anaweza kuitumia, ili akafanya kazi vizuri katika wilaya zetu za nchi yetu.

Jee Mhe. Waziri ana mpango gani wa kuitumia kamati pamoja na watendaji wake kutembea katika shehia zetu au katika mawilaya yetu kwa masheha na wazee maarufu, ili kuhakikisha kwamba jambo hili tunalielekeza nakulipiga vita isitokee katika nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa swali la Mhe. Mwenyekiti wa Kamati muhusika wa wizara ni kwamba mpaka sasa hivi tunandaa taratibu maalum mara tu baada ya mkutano wa utakapoisha Baraza,

kuwapangia mpango wa kwenda kutembelea katika sehemu ya shehia mbali mbali kukutana na watu wa shehia, kukutana na viongozi mbali mbali kujadiliana na kuona ni mikakati ipi itakayofanyika.

Wataanza kwa awali kwenye eneo moja wakishamaliza tutawapangia kwenye eneo jengine. Kwa hiyo, naomba ushirikiano wenu kwa kipitia chombo hiki viongozi wote kuanzia shehia mpaka ngazi za wilaya na mkoa waweze kutoa ushirikiano wa mali na hali kwa viongozi hawa kamati yetu itakapoanza kazi rasmi mara tu baada ya Baraza.

Nam. 14

Uanzishaji na Uimarishaji wa Viwanda Vidogo Vidogo

Mhe. Suleiman Sarhan Said (Kny. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa): – Aliuliza:

Kwa kujua umuhimu wa viwanda vidogo vidogo na kwa kuzingatia umuhimu wa ajira kwa vijana wa kujikwamua na umaskini, vijana wengi wamehamasika kujiunga na kujiendeleza katika maisha kwa kujishughulisha na kazi za utengenezaji wa sabuni za michi (vipande) na wengine kujishughulisha kwenye masuala ya kilimo cha viungo (*spices*).

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuviimarisha viwanda vidogo vidogo, ili vijana wengine wapate ajira na kukuza biashara hizo na serikali kupata pato lake.

(b) Serikali inachukua hatua gani kuwawezesha vijana hao wajasiriamali kwa kuwapatia nyenzo, ili waweze kuendelea na kazi hizo za ujasiriamali.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji (Kny. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko) - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa swali lake Nam. 14 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuhusu juhudi zinazooneshwa na vijana wengi kujikwamua na umaskini kwa kuanzisha na kuendesha miradi ya ujasiriamali, ikiwemo ya utengenezaji wa sabuni na kilimo cha viungo.

(a) Mhe. Naibu Spika, serikali inaendelea na taratibu za kusaidia viwanda vya wajasiriamali kwa kuvipatia mafunzo ya usarifu wa bidhaa, ufungashaji na matumizi ya njia bora za uzalishaji. Pia, wajasiriamali wazalishaji husaidiwa katika utafutaji wa masoko ya bidhaa zao kwa kushirikishwa katika maonesho mbali mbali ya ndani na nje ya nchi. Juhudi hizi zinafanywa na vyombo mbali mbali vya ndani na nje na watu binafsi, ambavyo mbali na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ni pamoja na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, na pia Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima (*ZNCCIA*).

Mhe. Naibu Spika, kwa lengo la kuimarisha mazingira bora ya usaidizi na maendeleo ya viwanda vidogo vidogo nchini. Serikali inaandaa taratibu za kuanzisha chombo maalum kitakachoshughulikia na kushirikiana pamoja na vijana itakuwa hili pia ni inajulikana kwa jina la Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati, Zanzibar (*SMIDA*).

(b) Mhe. Naibu Spika, ni kama nilivyosema katika kujibu kifungu (a) hapo juu, kuna wadau wengi wanaowasaidia wajasiriamali wakiwemo wenye viwanda vidogo vidogo. Wadau hao hutenga bajeti maalum kwa ajili ya misaada hiyo. Kwa upande wa Wizara yetu ya Biashara, Viwanda na Masoko katika mwaka huu wa fedha wa 2017/2018 zaidi ya shilingi milioni 400/= zimeshatengwa kusaidia miradi ya wajasiriamali.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Idara ya Viwanda katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 imewekwa bajeti ya jumla ya shilingi milioni 338,314,000/= kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali katika maeneo mbali mbali ikiwemo; kuandaa mafunzo ya mitindo ya mavazi, usarifu wa zao la mwani, kuimarisha uzalishaji wa dagaa na chumvi na kufanya utafiti wa asali.

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika na nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nataka kumuuliza Mhe. Waziri kwa sababu nimeona kuna baadhi ya bidhaa ambazo ziko Zanzibar ambazo za viwanda vidogo vidogo, lakini Zanzibar ina matunda na ina baadhi ya manukato. Je, Mhe. Waziri ana mpango gani wa kuweka viwanda vidogo vidogo kwa sababu sijawahi kuona Kiwanda cha *Juice* kinachotoka Zanzibar wala Kiwanda cha Manukato. Je, Mhe. Waziri ana mpango gani kuweka Viwanda vya Manukato na *Juice* kutoka Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji (Kny. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko): Mhe. Naibu Spika, katika kujibu swali hilo ningependa kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba serikali ina mpango kabambe wa kujenga viwanda vidogo vidogo na viwanda vya kati na lengo hasa litakuwa ni kusindika vyakula vyetu hapa, yaani *food process* tunajenga ambavyo vitatumia mali ghafi na mali ghafi hiyo itatokana na hapa nchini.

Kwa hivyo, natumai ataridhika akijua hili kwamba tutengeneza viwanda ambavyo vitashughulikia kwanza kusindika mali ghafi kutoka hapa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko itashirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Kilimo katika kuhakikisha kwamba tunajenga viwanda ambavyo vitapata malighafi kutoka hapa nchini. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 91

Gari za Matangazo Kupiga Kelele Njiani na Athari Zake

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Hivi karibuni kumekuwa na mtindo wa baadhi ya wafanyabiashara hasa za burudani na mawasilano kupita wakitoa matangazo kwa kutumia gari za mizigo midogo (*carry*) na gari

kubwa ambapo hufunga spika kubwa zinazofanya kelele njiani huku maeneo mengine yakiwa na skuli, hospitali na nyumba za ibada.

(a) Je, wizara inachukuwa hatua gani kudhibiti kelele hizo hasa ukizingatia Sheria ya Afya ya Jamii na Mazingira imekataza vitendo hivyo.

(b) Je, kwa vile kelele ni miongoni mwa mambo yanayohatarisha afya ya jamii, kwa nini hatua zinachelewa kuchukuliwa na vitendo hivyo vinaongezeka kila siku.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu swali langu kwanza naomba nifanye marekebisho juu ya kifungu namba 48 na 62 na badala yeke iingie katika *Hansard* 46 na 48.

Mhe. Naibu Spika, baada ya marekebisho haya sasa naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 91 na kabla ya kumjibu swali lake naomba kutoa maelelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, utoaji wa matangazo kwa kutumia gari barabarani na mitaani, utaratibu wake unasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa Nam. 7 ya mwaka 2014 chini ya Kifungu Nam. 46 na 48, Sheria ya Tawala za Mikoa Nam. 8 ya mwaka 2014 na Kanuni ya Matangazo ya Sheria Ndogo Ndogo ya Taasisi hizo. Aidha, Sheria Nam. 7 ya mwaka 2015 ya Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU) chini ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo nayo pia inahusika. Chini ya sheria hizo gari za matangazo zinatakiwa kuomba kibali Baraza la Manispaa.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi makini wa swali lake namba 91 lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika,

(a) Wizara inadhibiti kelele hizo kupitia mashirikiano ya pamoja kwa wanaotowa vibali, ambao ni Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ikiwemo Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri na Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu ya Wizara yetu, kwa sehemu ambazo biashara hiyo inafanyika.

(b) Hatua zinazo chukuliwa ni kwa wale wanaovunja Sheria, Masharti, Miongozo na Taratibu pamoja na ushauri wanaopewa. Hatua hizo huchukuliwa na Maafisa husika papo hapo inapobainika ili kulinda utulivu, amani na afya za jamii. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashimu Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri. Gari zinazopita katika sehemu ambazo haziruhusiwi kutangaza kama vile hospitali, mahakamani, skuli hata katika ukumbi wetu wa Baraza la Wawakilishi sehemu hizi hazitakiwi kuwa na bugudha au kelele kelele. Jee, wizara imechukuwa hatua gani ya dharura kuzungumza na Jeshi la Polisi kudhibiti matokeo hayo ikiwa wagonjwa wanapata kelele hospitali, mahakamani, skuli na hata hapa katika kumbi zetu za Baraza la Wawakilishi wakati tunaendelea na mkutano, hatua ya dharura imechukuliwa kunusuru matokeo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kuna sheria mbali mbali ambazo zinakataza matangazo katika sehemu kama ambazo amezitaja kwa mfano hospitali, skuli na hata sehemu za ibada.

Mhe. Naibu Spika, hatua ambazo tumekuwa tukuzichukua kwani na wao Jeshi la Polisi wanahusika na hili. Kwahiyo, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba hatua hizi tunakuwa tunazichukuwa na wao ni wahusika pia kuna sheria ambayo inawataka kuwafanya hivyo ahsante.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyoneza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Waziri katika jibu lake amesema kwamba wanadhibiti kelele kwa kushirikiana na Tawala la Mikoa.

a) Jee, ni kesi ngapi zilizojitokeza katika wizara hizo.
b) Hukumu gani ambazo wamehukumu watu hao au wafanyabiashara hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa idhini ....

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, nadhani Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ anataka kutoa majibu ya ziada naomba umuachie Mheshimiwa alikuwa na ziada ya lile Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Maryam Thani Juma swali lake la nyongeza. Lakini kabla sijamjibu swali hilo naomba nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameanza kuyatoa kuanzia kwenye swali mama na swali la nyongeza ambalo aliliuliza Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Baada ya maelezo hayo. Sasa naomba nichukuwe nafasi kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba mpaka sasa taasisi zetu hazijapata malalamiko kuhusu suala ambalo ameliuliza na hatuwezi kuwa na kesi ngapi sasa hivi kwasababu hatujapata malalamiko hayo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile niseme mtu yeyote anapokuja kuchukua kibaki na anapopewa ruhusa anapewa masharti kama alivyosema au alivyouliza Mhe. Jaku anapewa maelekezo kwamba kuna maeneo maalum haruhusiwi kama ni matangazo ya kufanya kelele akipita katika maeneo hayo kuweze kuendeleza na matangazo yake. Kwa mfano, kwenye maeneo ya hospitali, makahamani, Ikulu, Baraza la Wawakilishi na kwenye nyumba za Ibada huwa hawaruhusiwi kufanya hivyo, sasa pale anapofanya hivyo ni wajibu wa vyombo vya kisheria kuchukua mkondo wake na hivi

sasa tutakapogundua kwamba kuna tabia ya watu ambao wanafanya hayo kinyume na utaratibu basi serikali haitosita kuweza kuwachukulia hatua, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ nenda kakae. Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea na maswali na majibu, naomba niwatambulishe wageni wetu wa leo ni wanafunzi kutoka Skuli ya Sekondari ya Kibele jumla yao ni 37 wanaongozwa na walimu wao wawili pamoja na viongozi wa Serikali ya Wanafunzi ambao ni:

1. Mwalimu Mustafa Shafi Khatib
2. Mwalimu Mohammed Bakari Juma
3. Ndg. Kassim Issa Juma (ambaye ni Rais wa Serikali ya wanafuzi)
4. Ndg. Hadiya Haji Ali (ambaye ni Makamu wa Rais wa Serikali ya Wanafunzi)

Karibuni sana. (*Makofi*)

Nam. 73

Upotevu wa Mapato ya Mchanga

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Hivi karibuni kumeripotiwa upotevu mkubwa wa mapato ya mchanga ambapo gari 49 zimeripotiwa kukamatwa zikihusika na upotevu huo.

(a) Jee, ni kiasi gani cha mapato yaliyopotea kuhusiana na kadhia hiyo.

(b) Jee, mapato hayo yamepote vipi wakati watendaji wa Wizara ya Kilimo ndiyo wanaokusanya na kupeleka Benki ya Watu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 73 kama ifuatavyo lenye vipengele (a) na (b):-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kumetokea upotevu mkubwa wa mapato ya mchanga ambapo gari 49 yamehusika na upotevu huo. Kwa ujumla wake gari hizo ziliweza kuchukua jumla ya tani elfu tano mia tatu na arobaini (5,340) za mchanga kutoka shimo la Donge Chechele. Mchanga huo ulikuwa na thamani ya shilingi milioni thelathini na nane laki nne tisini na tano elfu na mia nne (38,495,400/-) za Kitanzania.

(b) Mhe. Naibu Spika, Serikali iliagiza malipo yote ya mchanga yafanywe moja kwa moja kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar katika kaunti maalum ya mchanga utekezaji wa agizo hilo tarehe 20/03/2017.

Mhe. Naibu Spika, kuanza kwa agizo hilo hakujajitokeza tatizo lolote katika kipindi cha mwanzo (Machi/April 2017) cha utekelezaji wake. Hatahivyo, kuanzia kipindi cha pili (April/Mei 2017) utekelezaji wa agizo hilo vitabu vya fedha vilivyopo katika Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka vilionesha tofauti ya fedha zilizomo katika stakabadhi zinazotolewa machimboni na hesabu zilizomo katika taarifa ya benki yaani *(bank statement),* jambo lilizua maswali mengi kwa watendaji wanaohusika na mahesabu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya uchunguzi wa awali ilibainika kwamba baadhi ya nyaraka za benki zilizotumika kufanyika malipo hazikuwa halisi na hazikuweza kuonekana katika taarifa za benki. Jambo lililoashiria kwamba baadhi ya wananchi walioukuwa wakichukua mchanga hawakuwa wakilipa katika akaunti ya mchanga ya benki ingawa kwa muonekano nyaraka hizo zilionekana kama halisi.

Mhe. Naibu Spika, kwahivyo mapato hayo yalipotea kwa kutumia nyaraka za kughushi katika kipindi ambacho hakukuwa na malipo yaliyokuwa yakipokelewa na watendaji wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri swali hili naona lina majibu mengine ya ziada lakini sijakusikia kuyasoma mwisho, halijamalizikia hapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu tulivyoambiwa tujibu kwa ufupi kwa hivyo nimeona hizi hazina haja ya kusomwa hapa na ndio maana nimefupisha jibu hilo.

Mhe. Naibu Spika: Wakati tayari limeshakuja hapa mbele yangu linatakiwa lijibiwe hivyo hivyo, ndio utaratibu tunaokwenda nao. Sasa sijui kama unalo hapo? Malizia kulijibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Nabu Spika, baada ya kubaini ubadhirifu huo wizara yangu ililiwasilisha suala hili katika vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumu Uchumi (*ZAECA*) kwa ajili ya uchunguzi na hatimae kufungua mashtaka. Uchunguzi wa shauri hii umekamilika na ameshakabidhiwa Mwendesha Mashtaka wa Serikali kuwafungulia kesi wahusika.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo Ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumu Uchumi imetufahamisha kwamba wahusika wakuu wa tatu (3) wa kesi ya msingi ambao ndio waliokuwa wanahodhi vitabu vya stakabadhi za benki na kuwauzia wenzao wamefunguliwa mashtaka Mahakamani na wale waliosalia wapigwe faini kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Nam.3 ya mwaka 2015 baada ya kukubali makosa yao na wakikataa kesi irudishwe Mahakamani. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, itabidi nizungumze kidogo kidogo ili Mhe. Naibu Waziri anipate vizuri kunisikiliza maana yake ananambia nakwenda mbio sana. Kwanza nimpongeze kwa kukiri kwa wizara yake imepoteza fedha nyingi za walipa kodi wa nchi hii, nikupongeze sana Mhe. Naibu Waziri. Nina swali moja tu dogo lenye vifungu (a) na (b).

a) Kwa majibu hayo serikali ilikuwa haijajipanga kusimamia rasilimali za mchanga mpaka wajanja wachache wameibia serikali fedha nyingi. Jee, suala la mchanga tumepigwa kama hivyo, likija suala la mafuta na gesi itakuwaje. Hivyo, uchunguzi umefanyika wa kina ilikuwaje ule mtandao wote wakakamatwa watu watatu tu, si kitu cha kusikitisha hicho.

b) Mhe. Waziri aliahidi kutwambia ndani ya chombo hiki wizara yake imejipanga katika kusimamia vizuri suala hili la rasilimali ya mchanga. Jee, haoni kuwa madudu hayo ameshindwa kutekeleza wajibu wake na ahadi yake katika chombo hiki. Tulipiga kelele sana suala hili akiwemo Mhe. Machano Othman Said, Mhe. Jaku Hashim Ayoub…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, umeshauliza kaa kitako.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza.

a) Mhe. Naibu Spika, uchunguzi umefanyika na umebaini watuhumiwa 49 ndio watuhumiwa ambao wameidanganya serikali, lakini wale ambao wamefanya vile vitabu ni watuhumiwa 3. Hivyo, tayari 27 wameshakiri makosa hayo na wameshalipa zile faini ambazo zimepangwa, na hao 23 ndio wamepelekwa Mahakamani kwa ajili ya hukumu.

b) Mhe. Naibu Spika, bado wizara inaendelea kujipanga na kwa sasa hivi iko vizuri na mapato yake yanapatikana kama kawaida. Ahsante.

Nam. 108

Malalamiko Juu ya Taratibu za Ukodishaji Mikarafuu

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kumekuwa na malalamiko kuhusu utaratibu wa ukodishaji wa mashamba ya karafuu, ambapo wananchi wenye mashamba yasiyo na waraka ulipotolewa na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kunyang'anywa na kukodishwa mtu mwengine na hivyo kuwakosesha haki ya kutumia mashamba hayo wake na watoto wa waliokuwa wamiliki wa mashamba hayo.

(a) Jee, ni sababu gani inayosababisha kwamba kuyakodisha mashamba hayo wake au watoto wa marehemu ambao walipewa shamba hizo hapo mwanzo.

(b) Ni lini hasa serikali itawakabidhi wananchi mashamba hayo, ili wayapande mikarafuu kwa maslahi yao na kuweza kuongeza uzalishaji wa karafuu.

(c) Jee, baada ya kukodisha kila shamba serikali hutenga asilimia ngapi ya fedha kwa ajili ya kuhudumia shamba.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 108 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake naomba kutoa maelezo ya jumla kuhusu ukodishwaji wa mashamba ya serikali ya eka kwa msimu wa mwaka wa 2017.

Nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba kuna malalamiko ya wananchi kuhusu ukodishwaji wa mashamba ya hayo ya eka tatu, lakini malalamiko hayo yanatokana na uelewa mdogo wa watu waliopewa kuhusu utaratibu mzima wa umiliki wa mashamba hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa mkataba wa matumizi ya mashamba hayo unampa mamlaka mume na mke kutumia shamba hilo katika kipindi cha uhai wao. Watakapokufa wote watoto wao wanatakiwa waombe serikalini na kupewa mamlaka ya matumizi jambo ambalo watu wengi hawakufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali lake kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Naibu Spika, imebainika kwamba kuna baadhi ya watu wasio waaminifu walikuwa wakiyahodhi na kuyaficha mashamba hayo na ndipo serikali ilipoamua mashamba yote yanayosimamiwa bila ya kuwa na mikataba rasmi ya umiliki yakodishwe na mapato yanayopatikana yaingizwe serikalini.

Mhe. Naibu Spika, ukodishaji wa mwaka huu watu wanaoyasimamia mashamba hayo wamepewa kipaumbele kuyakodi wao wenyewe na wapo ambao wamekubali kuyakodi kwa bei iliyofikia katika mnada na baadhi ya wengine wameamuru yakodishwe kwa watu wengine na wao wapewe kifuta jasho chao. Jumla ya mashamba 414 (174 Mkoani, 46 Chake-Chake, 110 Wete na 84 Micheweni) yameyakodishwa kwa wakulima wanayasimamia wenyewe. Pia, wakulima hao na wale wanaoyasimamaia mashamba ya eka yasiyokuwa na mikataba rasmi watapewa kifuta jasho kama serikali ivyoelekeza.

(b) Mhe. Naibu Spika, **s**erikali kwa kushirikiana na Ofisi za Mikoa na Wilaya, Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Masheha na wananchi mbalimbali inaendelea na kazi ya kuyatambua na kuyaratibu mashamba hayo. Baada ya kukamilika zowezi hili serikali itawakabidhi wananchi mashamba waliyoyaomba kwa mujibu wa taratibu. Kwa sasa wananchi wanaelekezwa kuyaomba mashamba hayo Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi wakati wizara inasubiri muongozo wa serikali wa kuyagawa mashamba hayo.

(c) Mhe. Naibu Spika, serikali inatenga pesa za kifuta jasho ambazo hugawiwa kwa wakulima wote wanaosimamia mashamba yaliyokodishwa na serikali ambayo hayana mikataba rasmi. Kifuta jasho hicho kinaanzia asilimia 10 hadi 40 ya kodi ya kila shamba.

Mhe. Naibu Spika, kulingana na huduma inayotolewa na mkulima anayesimamia shamba husika kufuatana na vigezo vilivyowekwa ambavyo ni (1) shamba hilo limesafishwa ndani ya mwaka husika na kuendelezwa kwa kupandwa mikarafuu na miti mingine ya kudumu (40%), (2) shamba hilo limeshasafishwa ndani ya mwaka husika lakini halikupandwa mikarafuu/miti mipya ya kudumu (30%), (3) shamba limesafishwa kwa

kipindi cha miaka miwili iliopita (20%) na (4) shamba ambalo halijasafishwa na wala kupandwa miti mipya lakini muhusika anailinda miti iliyomo (10%). Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii kwanza kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, leo ananijibu vizuri nimeridhika ahsante Mhe. Naibu Waziri. Lakini nina maswali yangu madogo nataka nikuulize, kwa kuwa tumekiri kwamba hayo mashamba tumeyakodisha kupitia Serikali za Wilaya, watu wa Usalama na Serikali za Mikoa zimeshirikiana tukayakodisha haya mashamba, na kwa sababu serikali imeshatoa maelekezo ya kuwapa kifuta jasho wale watu waliokuwa wameyaenzi hayo mashamba wengine wameyapanda.

a) Jee, nataka kujua tayari wameshatoa hiki kifuta jasho kwa wale wakulima ambao wanastahiki kupewa, na kama hawajatoa ni lini watatoa kifuta jasho hicho, ili wale wakulima waliokuwa na yale mashamba wazidi kuyaenzi na wapate *moral* wa kuyapanda wakati watakapopewa.

b) Ni kiasi gani cha fedha ambacho serikali imekikusanya kutokana na ukodishwaji wa shamba za eka tatu tu, wakiachilia mbali zile shamba kubwa zilizokuwemo chini ya Wizara ya Kilimo kama vile lile la Makuwe, Daya, Vikutani kule na mengineyo yaliyokuwa chini ya Wizara ya Kilimo. Ni hayo tu ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, kifuta jasho bado hatujaanza kutoa lakini tayari tumeshaandika barua kupeleka Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya utaratibu wa kuwalipa hawa wahusika waliokuwa wakisimamia mashamba hayo. Kwahiyo, itakapokuwa tayari watajua lini watapewa taarifa kupitia aidha redio au televisheni kutoa tangazo kwa wale ambao na hivyo tumewajazisha mkataba. Kwahivyo, wanajijua wenyewe na watakuja na mikataba yao kwa ajili ya kuwalipa fedha hizo. *(Makofi)*

b) Nafikiri kiasi cha shilingi bilioni 2.1 zinatarajiwa kukusanywa katika mashamba hayo ya eka tatu. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, labda nikufahamisheni muda hatuna na ndio maana nachukua swali moja la yule mwenye swali la msingi la nyongeza. Kwahiyo, wale ambao mnasimama kwa ajili ya maswali ya nyongeza ya ziada ya pili, ya tatu nitakuwa ninakata tuna maswali mengi na wenyewe mnazo *order paper* kuna maswali kama mengine matano yamebaki yanataka kujibiwa leo hii, tunamaliza saa nne hapa na baadaye jioni tunarudi kwa ajili ya kurudi kwa kufunga Baraza. Kwahiyo, mtanisamehe sana kwa leo lakini nitawapa tu wale ambao swali la msingi kuweza kupata swali la nyongeza. Ahsante.

Nam. 130

Upatikanaji wa Mbegu, Dawa na Maelekezo ya Ukulima Bora kwa Wakulima wa Mazao ya Mbogamboga

Mhe. Hidaya Ali Makame - Aliuliza:

Wakulima wa mazao ya mbogamboga walioko katika maeneo ya Kizimbani, Bumbwisudi, Mkanyageni, Miwani na kwengineko wangefaidika zaidi endapo huduma za ununuaji na uuzwaji wa mbegu, mbolea, dawa na maelekezo mengine ya ukulima bora wangeyapata kutoka pale chuoni kwa kupitia wahudumu wake kuliko kutoka sehemu nyengine za maduka ya vichochoroni.

(a) Jee, wizara inafahamu kwamba kupatikana kwa huduma hizo za uuzwaji wa mbegu, madawa na mbolea katika sehemu ya chuo kutaleta unafuu zaidi kwa wakulima kujua kuvitumia vitu hivyo kwa umakini zaidi.

(b) Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maliasili kwa kushirikiana na Wizara ya Afya haioni kwamba kutumia njia hiyo ingeweza pia kupunguza madhara na maradhi yanayosababishwa na wakulima hao kupitia mbogamboga na mazao mengine kuwekwa kemikali na kusababisha maradhi yakiwemo presha na sukari.

(c) Ni hatua gani za ziada zitachukuliwa na wizara kuweza kuwaelimisha wakulima na wananchi kwa ujumla, kuweza kujua kuzitumia na kuzifanyia kazi dawa ambazo zinatumika kuulia wadudu na kuimarisha mazao na mbogamboga, ili zitumiwe na zisiwaathiri watumiaji na vyakula hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 130 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Sera za Kilimo zimeeleza wazi kuwa biashara ya pembejeo na nyenginezo zimeelekezwa kwa sekta binafsi. Katika kutekeleza sera hizo, wizara iliwahamasisha wafanyabiashara na wakulima kuanzisha maduka ya pembejeo kupitia Mradi wa Ushirikishaji wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*PADEP*) katika miaka ya 2000 na mradi ulifanikiwaa kwa kuhamasiha wafanyabiashara na wakulima kuanzisha maduka kila wilaya. Hivyo, wizara haina mpango wa kuanzisha duka la pembejeo katika sehemu ya chuo. Lakini chuo kina programu za kuwafundisha wakulima kilimo bora ikiwemo matumizi bora ya pembejeo.

(b) Mhe. Naibu Spika, wizara inaamini kuwa afya ya wakulima ni muhimu. Hivyo, kuhusu masuala ya afya, wizara imekuwa inashirikiana na wizara husika. Aidha, wizara kupitia idara husika inaelimisha wakulima matumizi bora ya dawa za kilimo.

(c) Mhe. Naibu Spika, hatua ambazo zinachukuliwa na zitaendelea kuchukuliwa ni kuwafundisha na kuwasisitiza wakulima wafuate maelekezo ambayo kwa kawaida kila aina ya dawa ya kuuliwa wadudu inakuwa na maelekezo ya matumizi pamoja na muda wa kusubiri kabla ya kuvuna. Ahsante.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo tangu jana ananijibu lakini kama yananivunja moyo hivi.

a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli wizara haina bajeti ya maendeleo ndani ya Chuo cha Kilimo, lakini pia wizara haina mpango wa kuanzisha maduka haya ya hizi dawa na mbegu. Lakini jee, Mhe. Naibu Spika, kama wizara ina maeneo makubwa ndani ya Chuo cha Kilimo Kizimbani, ina mpango gani wa kuwapa hawa wakulima binafsi au wafanyakabiashara binafsi, ili wakaweza kujenga maduka pale karibu na chuo kwa ajili ya kuwahamasisha zaidi wale wakulima wanapokuja kununua zile dawa wakakutana na wale wahusika pale ndani ya chuo wakaweza kuwafahamisha na yale matumisi mengine ya dawa hizi za mbogamboga na matunda.

b) Kama kuna mashirikiano na wizara jee, hawaoni kwamba sasa ipo haja ya kupita humo masokoni labda kwasababu tunaonekana kwamba dawa haitumiwi ipasavyo kwa wakulima. Mkulima anakwenda kununua dawa saa kumi anapiga mbogamboga saa kumi na mbili jioni anaenda kuikata anauzia wananchi. Jee, hili tatizo halionekani na wizara na kama linaonekana, kuna mpango gani binafsi wakuchukuliwa ndani ya wizara hizi mbili kushirikiana wakalihakikisha hili suala linafanyiwa kazi na hizi dawa hazitumiwi ovyo ovyo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

a) Mhe. Naibu Spika, eneo hili hatutaweza kuwapatia watu hawa kwani eneo hili ni eneo la utafiti tunalitumia kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali.

b) Matumizi ya dawa kama tulivyosema tunajaribu kuwafundisha wakulima muda gani wa kupiga dawa na muda gani wa kuvuna mavuno yale. Mhe. Naibu Spika, napenda kumwambia Mhe. Mwakilishi kwamba labda kwenye hili tusaidiane pamoja kuwafundisha na kutoa taaluma ili wasirudie yale makosa ambayo wanarudia. Lakini kwa upande wa wizara tayari tunafundisha na tunaelimisha kwamba ni muda gani upige dawa na muda gani uanze kuvuna mavuno. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, nataka niongezee majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri. Baada ya kuona tatizo hili la *chemical* zilizomo katika mazao mbalimbali, taasisi zetu za utafiti imefanya utafiti wa kutumia mwani, kutumia mwarubaini kuweza kutibu baadhi ya maradhi hasa kwenye mbogamboga. Mhe. Naibu Spika, nawaomba wananchi pamoja na wawakilishi waende kwenye mabanda ya maonesho wakaone namna gani tunaweza tukatumia miti yetu ya asili, majani yetu ya asili ambayo yanaweza kutibu hasa katika mazao ya mbogamboga.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba tufanye juhudi hiyo tukaone ili tuweze kuwafahamisha watu wetu. Nimeona mashamba mengi ya nyanya kwa mfano watu wametumia mwarubaini na baadhi ya karafuu kidogo, wamechanganya na tangawizi kidogo na hatimae unaweza kutibu maradhi ambayo yanapatikana kwenye nyanya. Kwahiyo, naomba waende wakapate taaluma hiyo wataweza kuona kiasi gani tunaweza tukapunguza matumizi ya *chemical*.

Nam. 64

Hali ya Maradhi ya Kichocho Kisiwani Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Mnamo tarehe 20/7/2017, vyombo vya habari mbalimbali, likiwemo Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) vimeripoti kuwa maradhi ya Kichocho Kisiwani Pemba yapo juu.

(a) Ni sababu gani zimepelekea maradhi hayo yenye athari mbaya kwa jamii kuongezeka kwa kasi Kisiwani Pemba.

(b) Ni lini zowezi la ugawaji dawa Kisiwani Pemba litafanyika, ili kudhibiti kasi ya ongezeko la maradhi hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 64 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nafarajika sana kulieleza Baraza lako Tukufu kwamba Maradhi ya Kichocho Zanzibar hayaongezeki yamepungua na yanaendelea kupungua Unguja na Pemba kutoka asilimia 60, kwenye miaka ya 80 hadi asilimia 1.7 kwa mwaka huu 2017 kwa tathmini haya ni mafanikio makubwa.

Hatahivyo, kuna baadhi ya shehia Unguja na Pemba bado maambukizi ya kichocho yako juu, hii inatokana na kuwepo kwa mito ya maji na madimbwi mengi katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kupitia Kitengo Maalum cha Kichocho kwa mashirikiano na Kamati za Masheha na Kamati za Afya zilizo katika shehia tunatoa elimu kwa wananchi juu ya athari za kichocho, umuhimu wa kujenga na kutumia vyoo, pamoja na kutumia maji safi na salama kwa shughuli za kijamii kama kunywa, kukoga, kupikia na kuacha kutumia maji ya mito ambayo ni vyanzo vikubwa vya kuzalisha vimelea vya maradhi hayo.

Wizara pia ina utaratibu maalum ya ugawaji wa dawa kwa wananchi kila nyumba mara 2 kwa mwaka, yaani kila ifikapo mwezi wa Mei na mwezi wa Oktoba pamoja na kunyunyiza dawa kwenye madimbwi na mito, ili kutokomeza makonokono yenye vimelea vya maambukizi haya.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasihi wananchi waache tabia ya kudharau kula dawa za minyoo, wakati wafanyakazi wetu wanapopita majumbani kutoa dawa hizo, kwani tuna taarifa kwamba baadhi ya wananchi wanazipokea na kuziacha bila ya kuzila au kuzitupa kwa visingizio mbali mbali.

Mwisho nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wa wananchi kutumia nafasi zao kuwahamasisha wananchi kula dawa za kichocho zikitolewa majumbani kwa kulinda afya zao. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri vyombo vya habari vimeripoti maradhi ya kichocho Kisiwani Pemba yako juu na hayo si maneno yangu ni vyombo vya habari vilitoa tarehe 20 mwezi wa Julai. Anaweza kutwambia ni maeneo gani Pemba yaliyoko juu kwa maradhi haya na kwa upande wa Unguja ni maeneo gani ili wananchi wapate kufahamu na wachukue jitihada kama kuna mito waanze kuepukana nayo tusubiri maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, ni kweli vyombo vya habari vilitangaza kuweko kwa kichocho Kisiwani Pemba, lakini ni kwa baadhi ya shehia sio sehemu zote. Kwa Pemba kichocho kinasumbua zaidi katika shehia zifuatazo:

Shehia ya Kinyasini
Shehia ya Chambani
Shehia ya Uwandani
Shehia ya Shumba Viamboni
Shehia ya Wambaa
Shehia ya Vitongoji
Shehia ya Ziwani
Shehia ya Pujini na
Shehia ya Mgogoni.

Mhe. Naibu Spika, lakini katika shehia nyengine zilizobaki ziko salama na hakuna maambukizi makubwa ya vimelea hivi vya kichocho.

Nam. 89

Kuendelea kwa Ubovu wa *Lift* ya Hospitali ya Mnazimmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Kwa muda mrefu sasa karibu miezi mitatu "*lift*" ya Hospitali ya Mnazimmoja imekuwa haifanyi kazi na kusababisha usumbufu kwa wagonjwa wanaohitaji kupandishwa juu. Hali hiyo pia inawasumbua jamaa wa wagonjwa ambao wanalazimika kumbeba mgonjwa kwenda naye juu kwa kutumia ngazi.

(a) Jee, ni kwa nini "*lifti*" hiyo kwa muda mrefu imeachwa bila ya kutengenezwa.

(b) Jee, gharama kiasi gani zinahitajika kuifanyia matengenezo "*lift*" hiyo na kwa nini serikali haitafuti fedha hizo haraka, ili "*lift*" hiyo ikatengenezwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 89 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli *lift* ya Hospitali ya Mnazimmoja ilikuwa haifanyi kazi takriban miaka mitatu, ambapo iliharibika kutokana na kutofanyiwa *service* za kawaida. Pia kulikuwa na deni la shilingi 20,945,000/= ambalo lilichelewa kulipwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa sasa *lift* ya Hospitali ya Mnazimmoja inafanya kazi vizuri baada ya deni hilo kulipwa pia hospitali kuingia mkataba na Kampuni ya *OTIS*, ili kuifanyia matengenezo pamoja na *service lift* hiyo na kuepusha kwa kuharibika mara kwa mara na kuleta usumbufu kwa wananchi hususan wagonjwa ambao ndio watumiaji wakubwa wa *lift* hiyo. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri jana, juzi nilimueleza kabla ya kujibu swali afanye utafiti kwanza Mheshimiwa. Saa 11:07 niko Hospitali ya Mnazimmoja alfajiri na hayo ninayozungumza Mwenyezi Mungu ananisikia kama nazungumza uongo kwenda kuhakikisha hiki ninachozungumza ni sawa sawa? *Lift* moja imewekewa ma-*grill*, moja nikenda kuuliza haifanyi kazi, leo Mheshimiwa wananchi wanatusikiliza chombo hiki muhimu, anakuja kunijibu hivi Mhe. Naibu Waziri. Kwa masikitiko makubwa naomba afute kauli yake.

Mhe. Naibu Spika, *lift* haifanyi kazi twende zetu mguu kwa mguu mimi na yeye hivi sasa. Saa 11:07 alfajiri sijaswali mimi niko Hospitali ya Mnazimmoja, leo yanakuja majibu *lift* inafanya kazi halafu kwa nini niashirie. Mhe. Naibu Spika, ...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim nimekunyanyua kwa ajili ya kuuliza swali la nyongeza sio maelezo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Naibu Waziri aombe radhi analidanganya Baraza na uthibitisho ninao.

Mhe. Naibu Spika: Hapana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, sio hapana Mhe. Rais anatusikia kazi tunayoifanya hii anaiona wanamuangusha Mhe. Rais hawa watu. *Lift* anakuja kusema inafanya kazi wakati haifanyi kazi, haiwezekani. Mheshimiwa haiwezekani hili Rais anafanya kazi sote tunaiona.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim naomba ukae. Mhe. Naibu Waziri una maelezo yoyote.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake, sio swali naomba nitoe maelezo. Mhe. Naibu Spika, yeye anasema amekwenda leo asubuhi saa 11:00, lakini nimeondoka jana usiku na *lift* moja inafanya kazi kama kawaida. Hapa aliuliza *lift* sikupaswa kutolea maelezo *lift* zote mbili aliuliza *lift* kwa hiyo *lift* ambayo inafanya kazi kwa muda mrefu ni hiyo ambayo nimeieleza na ni nzima na kama kunatakiwa ushahidi atoke mwakilishi yeyote sasa hivi aende akapande kwenye *lift*.

Mhe. Naibu Spika, lakini nilikuwa naomba nitoe tahadhari kidogo na maelezo kwa Waheshimiwa Wawakilishi. Mhe. Jaku Hashim Ayoub leo alfajiri kweli amekwenda katika

Hospitlai ya Mnazimoja na naomba Waheshimiwa Wajumbe mkienda katika Hospitali ya Mnazimmoja au taasisi yoyote kila pahala pana utaratibu wake. Mheshimiwa kadhalilishwa sana kitu ambacho sikupenda. Hospitali ya Mnazimmoja kuna walinzi na ni walinzi makini ambao wamepewa mafunzo wanalinda katika sehemu ile. Mhe. Mjumbe alichokifanya kaenda hospitali bila ya taarifa na ni kabla ya wakati wa kuangalia wagonjwa, kilichomfika walinzi wamemdhibiti wamemkatalia kuingia katika hospitali hiyo kwa sababu wana haki na wajibu wa kufanya hivyo. Nawaomba Waheshimiwa mara nyengine yoyote wanapohitaji...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu, alipotosha Baraza mimi nimeruhusiwa...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub naomba sana usisimame, tafadhali kiheshimu hiki chombo na niheshimu mimi ambaye niko hapa, kama sijakuruhusu kusimama usisimame.

Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na swali jengine la Nam. 90 Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Nam. 90

Ubovu wa Mashine ya Kuchomea Taka Hospitali ya Mnazi Mmoja

(Mheshimiwa aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 121

Deni la Shirika la Ndege la Tanzania (*ATC*)

Mhe. Machano Othman Said – Aliuliza:

Katika miaka ya 2005-2010 wakati Shirika la Ndege la Tanzania (*ATC*) lilipoyumba kiuchumi hadi kuchukuliwa na Shirika la Ndege la Afrika ya Kusini (*SAA*), Shirika hilo la *ATC* liliacha deni kubwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(a) Kwa kuwa hivi sasa *ATC* imeimarika kibiashara. Jee, serikali imejipanga vipi kudai deni hilo.

(b) Ni kiasi gani cha deni hilo ambalo lipo na linatambuliwa rasmi.

(c) Jee, katika Bodi ya Wakurugenzi ya *ATC* yupo mjumbe yeyote kutoka Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 121 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, serikali kwa kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege tayari imeshaanza mazungumzo na Shirika la Ndege la Tanzania (*ATC*), ili shirika hilo liweze kuilipa mamlaka deni lake inaloidai.

(b) Mhe. Naibu Spika, mamlaka inalidai Shirika la Ndege la Tanzania jumla ya shilingi 241,141,778 ikiwa ni deni au ni ada za *"Landing Fee".*

(c) Mhe. Naibu Spika, katika Bodi ya Wakurugenzi ya *ATC* hakuna mjumbe yoyote kutoka Zanzibar kwa hii bodi iliyotangazwa karibuni. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini nina swali moja la nyongeza. Shirika la Ndege la Tanzania (*ATC*) sawa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (*CCAA*) na Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Tanania (*TCMA*), haya ni Mashirika ya Muungano ambayo yalitokana na Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika na kwa muda mrefu mashirika haya yalikuwa na Mwakilishi wa Zanzibar katika Bodi ya Wakurugenzi.

Jee, ni sababu zipi zilizopelekea bodi mpya ya *ATC* kutokuwa na mjumbe kutoka Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Machano Othman Said swali lake la nyongeze. Ni kweli hivi karibuni tu sisi pamoja na Kamati ya Ardhi na Mawasiliano tulikuwa Dar es Salaam, katika ziara yetu ile tulikutana na Bodi ya *ATC* pamoja na waziri husika, walikiri hili tatizo na wakaahidi kwamba kwa hapo baadae hili tatizo halitorejewa tena, ndio maana karibuni tu hata ilipoletwa ile *first draft* ya Mswada wa Sheria kuhusiana na Uanzishaji wa Shirika la Simu.

Pia walikuja na wakapata maoni yetu na katika mswada ule wamependekeza kwamba lazima katika wajumbe wa bodi angalau mmoja atoke Zanzibar na sisi tukaleta maoni yetu zaidi, nafikiri serikalini tutatoa maoni yetu zaidi kuhusiana na hili. Kwa hivyo, wamekiri na hili suala ni kweli limetokezea kwa hiyo, hapo baadae nina imani halitotokea tena ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 128

Ubovu wa Barabara Zilizoathirika kwa Mvua zilizonyesha hivi Karibuni

Mhe. Hidaya Ali Makame - Aliuliza:

Kwa kuwa mvua zilizonyesha hivi karibuni katika msimu wa masika zimepelekea baadhi ya barabara nyingi za hapa nchini kuharibika vibaya na nyengine kutopitika kabisa. Pamoja na hali hiyo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imefanya juhudi mbalimbali za kuzikarabati baadhi ya barabara hizo na napenda kuchukua fursa hii kuipongeza serikali kwa hatua hiyo. Hatahivyo, baadhi ya barabara bado zina matatizo makubwa ya mashimo ikiwemo barabara inayotokea Unguja Ukuu Kiembeni hadi Uzi Ng'ambwa, ambapo barabara hii ina matatizo makubwa kwa hivi sasa na wananchi wa maeneo hayo hufanya juhudi za kufanya ukarabati kwa nguvu zao wenyewe.

(a) Jee, wizara imechukua hatua gani za kumalizia pale wananchi waliposhindwa kumalizia kwa kuweka angalau zege katika eneo hilo.

(b) Kuna utaratibu gani wa wizara kuimarisha miundombinu ya barabara katika vijiji ambavyo vina mazingira ya vivuko kikiwemo kijiji cha Uzi na kwengineko.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 128 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na barabara aliyoitaja Mhe. Mwakilishi, barabara ya Unguja Ukuu Kiembeni hadi Uzi Ng'ambwa inaunganisha Kisiwa cha Unguja na Kisiwa cha Uzi, barabara hiyo yenye urefu wa kilomita zisizopungua 2 inapitia baharini na haikuathiriwa na mvua zilizonyesha mwezi wa April - Mei, 2017 kwa kufanya mashimo kama alivyosema Mjumbe. Wizara yangu inatambua uwepo wa barabara hiyo na juhudi wanazochukua wananchi kwa kushirikiana na wizara yetu ni juhudi ambazo zinabidi kupongezwa kwa dhati na wananchi hao wa Uzi - Ng'ambwa, kwa moyo wa kizalendo wa kujitolea kwa kufanya matengenezo ya mara kwa mara barabara hiyo ili kupitika kwa wepesi wakati serikali ikitafuta fedha ya kujenga au kuweka miundombinu itayoonekana inafaa ya kuwaunganisha wananchi wa Uzi na Unguja Ukuu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imekuwa ikiwapatia nyezo (saruji, zana ndogo ndogo za ujenzi) wananchi hao walioamua kujitolea kwa kuifanyia matengenezo barabara hiyo kwa kujaza mawe na uwekaji wa kokoto na zege kama walivyopendekeza kwa kushirikiana na Idara ya *UUB* na ndiyo maana matengenezo ya barabara hiyo ndipo yalipofikia pale.

(b) Wizara inatafuta fedha zaidi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na sanifu ya aina ya miundombinu itakayojengwa na kuwekwa ili kuwawezesha wananchi wa Kisiwani Uzi kuwasiliana na wenzao wa Kisiwa cha Unguja kwa salama na rahisi. Kuhusiana na suala la kujenga miundombinu ya barabara kisiwani humo, wizara imelichukua na italifanyia kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi tena kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanaweza yakawapa moyo wananchi wa kijij cha Uzi-Ng'ambwa wakaweza kuona kweli serikali yao inawajali.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri jee, yeye akiwa kama ni Naibu Waziri wa Miundombinu alishawahi kwenda kwenye kijiji hiki cha Uzi-Ng'ambwa. Kama keshawahi kwenda jee, kuna utaratibu gani yeye kama wizara kuweza kuchukua angalau lile

shindilio kila baada ya mwezi kuweza kulipitisha mule kwenye ile njia, ili kupunguza yale mawe makali ambayo yanachongeka kwa ile bahari kali inayokuwepo pale baada ya maji kujaa, ili zile gari zinazokwenda na kurudi ziweze kupita kwa vizuri na zile baskeli za wale wananchi zipite kwa vizuri bila ya kupasuka mipira kila siku.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu tena Mhe. Hidaya Ali Makame. Kama nilivyosema awali mimi juzi tu nilikuweko Uzi-Ng'ambwa nilikwenda kuiangalia hiyo barabara. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Mwakilishi ambaye ameanza kuchukua hatua ya kuweka kifusi pamoja na mbunge mwenzake kule ukishavuka Uzi-Ng'ambwa.

Nilikwenda nikaonana na ile kamati ambayo yule mtengenezaji wao mkuu Shaa anaumwa sasa hivi, nimekutana na kamati ile na tumepanga kwamba tuhakikishe sasa kwa sababu tunatia zege tushatoka hatujafika kwenye mito ile miwili mikubwa, tukifika pale wenyewe wamenipa ushauri na ushauri huo nimeuchukua na nitaupeleka wizarani. Lakini kama anavyosema sisi tutahakikisha kwamba ile barabara kila wakati tunaitengeneza, kwa sababu pale wenyewe tunasema mkondo wa maji kwenye mito miwili pale maji yanapita kwa kasi wakati wa bamvua kubwa kwa hiyo inabidi lazima tutafute utaalamu zaidi wa kuhakikisha kwamba zile kokoto zitazotengenezwa pale zitakaa kwa muda mrefu.

Vilevile, bado tuna uamuzi wa baadae ambao tunaanza kufanya upembuzi yakinifu kutoka Makine huku Unguja Ukuu ambako iko Kambi ya KMKM na zilipopita nguzo za umeme, ili kuangalia kwamba namna gani tutajenga daraja japo kwa baadae. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawajali wananchi wake na itahakikisha kwamba miundombinu hii ya barabara inaipeleka sehemu yoyote pale kwa ajili ya kurahisisha wananchi wake, ili kuendelea na shughuli za maendeleo ili tufikie katika maendeleo ya kati kama ilivyokusudiwa katika Ilani yetu ya Uchaguzi wa CCM. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze muuliza swali hili Mhe. Hidaya Ali Makame kwa kufuatilia mambo ambayo yana adha wakati wa mvua ambazo zinatokea katika nchi yetu. Lakini swali langu liko hapa Mhe. Naibu Spika.

Tumeshuhudia wakati wa mvua nyingi Zanzibar barabara zetu huwa zinakatika pembeni mwa barabara kukosekana kingo au kujengewa vile vikuta vidogo vidogo ya kunusuru.

Jee, kwa kuzingatia hilo wizara ina mpango gani wa makusudi kuzijengea barabara zetu kingo za pembeni au vikuta vidogo vidgo, ili kuzinusuru wakati wa mvua, hasa barabara zetu nyingi lakini naichukulia zaidi ya kutoka Mwanakwerekwe hadi Fuoni na nyenginezo. Wizara ina mpango gani wa kuondoa adha hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukuwa nafasi hii kumjibu Mhe. Ali Suleimana Ali swali lake kama ifuatavyo:

Ni kweli tunajua hasara inayotokezea hivi sasa. Karibuni kabisa tumeiona Pemba athari hiyo, kwa hiyo, sehemu ambazo tuna uwezo wa kujenga *stone peach*, ili kuzuia athari kama hizo watajega *stone peach* na sehemu ambazo tunahisi tunahitaji mitaro basi tutahakikisha kwamba tunajenga mitaro ili kuhakikisha zile barabara hazihathiriki kutokana na gharama kubwa tunayotumia katika kutengeneza barabara zile. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Kufuta Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya Mwaka 1984 na kutunga Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 2017

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais): Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba Mswada wa kufuta Sheria ya Uchaguzi Nambari 11 ya Mwaka 1984 na kutunga Sheria mpya ya Uchaguzi ya Mwaka 1917 na masuala mengine yanayohusiana na hayo naomba kusoma kwa mara ya kwanza. (*Makofi*)

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar na Kuweka Vifungu vya Usajili na Mambo mengine yanayohusiana na hayo

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar na kuweka Vifungu vya Usajili na mambo mengine yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya kwanza. (*Makofi*)

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati Zanzibar

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi (Kny. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko): Mhe. Naibu Spika, naomba Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati Zanzibar pamoja na Kuwezesha Uzalishaji na Uendeshaji wa Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo, kusomwa kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Mswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali na Kuweka Masharti Bora ndani yake na Mambo Mengeine Yanayohusiana na Hayo

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, naomba kuweka Mswada wa Marekebisho ya Sheria mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora ndani yake na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo kwa kusomwa mara ya kwanza. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu. Waheshimiwa Wajumbe, shughuli za asubuhi hii tumezimaliza kutokana na *order paper* yetu na kama mnavyofahamu leo itakuwa ni siku ya kufunga Baraza letu, katika Baraza letu hili la Tisa, Mkutano wa Saba.

Mhe. Spika atakuja jioni kwa ajili ya kufunga Baraza hili, atakuwepo hapa kwa ajili ya kufunga Baraza hili. Kwa hiyo, ninawashukuru sana kwa ushirikiano wenu pamoja na usikivu wenu ambao mmeuonesha wakati wote ambapo tulikuwa na mimi pamoja na wenyeviti tunaendesha vikao hivi.

Sasa niseme tu kwamba nasitisha shughuli hizi za leo asubuhi mpaka mchana saa 11 jioni. Ahsanteni sana.

(Saa 5:02 asubuhi Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11: Jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Ahsanteni Waheshimiwa Wajumbe leo tutakuwa tumefikia mwisho wa shughuli zetu naomba nichukuwe nafasi hii sasa kumkaribisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili sasa aje atoe hotuba yake. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais karibu sana. (*Makofi*)

HOTUBA YA MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR YA KUAKHIRISHA MKUTANO WA SABA WA BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, awali ya yote naomba tumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwenye wingi wa rehma Muumba mbingu na ardhi na vilivyo ndani yake kwa kutujaalia uhai kuwa wazima na afya njema tukaweza kufanikisha kwa ufanisi mkubwa shughuli zote tulizopangiwa na Baraza letu tukufu kuanzia tarehe 27 Septemba hadi leo tarehe 12 Oktoba, 2017, siku ambayo tunaakhirisha Baraza hili.

Mhe. Spika, Napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Spika kwa umahiri na uongozi wako imara wenye busara na heshima nyingi wa kuendesha vikao vyetu katika mazingira ya kuelewana, kupendana, kusaidiana, kushirikiana na kushauriana. Shukrani zangu pia ziwafikie Wenyeviti wote wa kamati 7 za kudumu kwa kazi zao nzuri na za kupigiwa mfano.

Pia shukrani zangu ziwaendee Katibu wa Baraza na wasaidizi wake wote waliokuwa chini yake kwa mashirikiano makubwa wanayotupatia siku zote katika kutekeleza shughuli zetu za Baraza. Shughuli zetu hizi za Baraza letu tukufu zimefanikishwa na watu wengi wakiwemo waandishi wa habari, wataalamu wa lugha za alama na wananchi waliokuwa wakitusikiliza. Hivyo basi naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa wote hao.

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein kwa namna anavyosimamia na kufuatilia utekelezaji wa ahadi zake. Nyote ni mashahidi ziara alizozifanya katika Mikoa na Wilaya zote za Unguja na Pemba pamoja na Taasisi za Serikali zimesaidia kuamsha ari za watendaji wetu serikalini. Aidha nampongeza tena Mhe. Rais kwa uteuzi alioufanya hivi karibuni kwa watendaji mbali mbali wa serikali kwa lengo lile lile la kuongeza ufanisi wa kusimamia vyema shughuli zetu za kiserikali. (*Makofi*)

Mhe. Rais ameonyesha imani kubwa juu ya wale wote aliyowateua kuwa watamudu kazi zao barababa. Ni imani yangu kwamba watafanya kazi zao kwa kufuata kauli mbiu ya Tubadilike, tusifanye kazi kwa mazoea. Naamini wataifuata kwa dhati kaulimbiu hiyo.

Mhe. Spika, pia naomba tumpongeze kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa jinsi anavyosimamia vizuri rasilimali za nchi yetu ili ziwanufaishe walio wengi hapa nchini badala ya wajanja wachache. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inamuunga mkono kwa dhati kwa jitihada zake hizo kwani tunaelewa si muda mrefu watanzania wataanza kunufaika na rasilimali zao. Tumeibiwa siku nyingi lakini sasa iwe basi.

Mhe. Spika, katika mkutano huu wa saba wa Baraza lako tukufu Wajumbe wako wameuliza na kupatiwa majibu maswali ya Msingi mia moja na ishirini na nane (128) na maswali ya nyongeza mia mbili na hamsini na moja. Wingi huu wa maswali katika kipindi kifupi cha Baraza unaonyesha umakini walionao Wajumbe wako katika kufuatilia kwa karibu kero za wananchi wanaowawakilisha. Aidha

napenda kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa kuyatolea ufafanuzi wa kina maswala yote ya msingi na yale ya nyongeza yaliyoulizwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mkutano wetu huu umepokea na kujadili na hatimaye kupitisha kuwa sheria Miswada Miwili (2) kama ifuatavyo:-

1. Mswada wa Sheria ya kufuta sheria ya Mahakama ya Kadhi Namb. 3 ya mwaka 1985 na kuanzisha upya Mahakama ya Kadhi na kuweka masharti mengine yanayohusiana na hayo.
2. Mswada wa Pili ni mswada wa Sheria ya kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na kuweka mambo mengine yanahusiana na hayo.

Mhe. Spika, kuanzishwa upya kwa Mahakama ya Kadhi nchini kutasaidia kuondosha kasoro nyingi zilizolalamikiwa na wananchi wetu hasa kwenye suala la utoaji haki. Mapungufu mengine tuliyoyaondoa ni yale ya kuonekana Mahakama ya Kadhi kama Idara ya Mahakama kuu. Kwa hivyo mswaada huu utakapokuwa sheria Mahakama ya Kadhi itakuwa inajitegemea jambo ambalo ni muhimu sana katika utoaji wa haki.

Mhe. Spika, mswada wa Sheria ya kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara umekuja wakati muwafaka ambapo mwelekeo wetu ni kuwa na uchumi wa kipato cha kati kwa kipindi kifupi kijacho. Tuna imani kubwa Baraza jipya la Taifa la Biashara litasaidia kuirejeshea hadhi yake Zanzibar ya kuwa kituo kikubwa cha biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki. Hata hivyo, ushauri wangu kwa wale Wajumbe watakaobahatika kuingia katika Baraza hili kutokusahau pia maslahi ya wananchi wetu walio wanyonge katika mfumo mzima wa uratibu wa Biashara nchini.

Mhe. Spika, Baraza letu tukufu pia lilipangiwa kupokea ripoti 15 za utekelezaji za mawizara zinazotokana na maelekezo ya kamati kwa mwaka 2016/2017 kama ifuatavyo: -

i. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2016/2017.
ii. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2016/2017.

iii. Ofisi ya Rais, Katiba, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa mwaka 2016/2017.

iv. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora, na Idara Maalum ya mwaka 2016/2017.

v. Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya mwaka 2016/2017.

vi. Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya mwaka 2016/2017.

vii. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya mwaka 2016/2017.

viii. Wizara ya Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2016/2017.

ix. Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya mwaka 2016/2017.

x. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya mwaka 2016/2017.

xi. Wizara ya Afya imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya mwaka 2016/2017.

xii. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2016/2017.

xiii. Wizara ya Fedha na Mipango imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2016/2017.

xiv. Wizara ya Fedha na Mipango imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maelekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) kwa mwaka 2016/2017. na mwisho,

xv. Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira imewasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (*ZAWA*) ya mwaka 2016/2017.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru sana kwa mara nyengine tena Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuchangia mambo muhimu wakati wa majadiliano ya ripoti hizi. Serikali inaahidi kuyafanyia kazi maelekezo yao. Tunaamini na

tutaendelea kuamini na kuthamini michango iliyotolewa kwani ndiyo iliyozikamilisha ripoti zetu kukidhi matarajio ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hivi sasa nchi yetu imo katika msimu wa zao la Karafuu ambalo ni zao mama la uchumi wa Zanzibar. Serikali kwa upande wake inawataka wananchi kuziuza karafuu zote Serikalini na kujiepusha na magendo ambayo yanahujumu uchumi wetu. Serikali haitomvumilia mtu yoyote anayefanya biashara ya magendo ya karafuu kwa kuzitoroshea nchi jirani. Ili tufanikiwe kuokoa zao letu la karafuu nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi kuwahamasisha wananchi wetu kushiriki katika uchumaji wa karafuu zetu na kuziusha katika Shirika la Biashara.

Mhe. Spika, napenda kuipongeza sana *Task Force* yetu huko Pemba pamoja na Vikosi vyetu vya Ulinzi hasa KMKM pamoja na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wetu kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kulilinda zao letu hilo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, uhaba wa vikalio mashuleni kuanzia shule za maandalizi, msingi mpaka sekondari bado imekuwa ni changamoto kubwa katika sekta ya elimu hapa nchini. Hii inadhihirishwa na *data* tulizonazo ambazo zinaonesha mpaka kufikia mwezi Machi 2016 jumla ya wanafunzi 188,060 sawa na asilimia 56.4% ya wanafunzi wote katika skuli za Serikali hawana vikalio. Idadi hii ilikuwa ni sawa na upungufu wa madawati 47,448 kwa wanafunzi wa ngazi ya msingi na viti 45,716 na meza 45,716 kwa wanafunzi wa ngazi ya elimu ya Sekondari.

Hadi kufikia mwezi Julai 2017, Jumla ya Madawati 6,326, Viti 3,512 na Meza 2,892 vimepatikana ambavyo vimesambazwa katika skuli mbali mbali za serikali. Jumla ya wanafunzi 25,382 wameweza kupata vikalio na hivyo kupunguza idadi ya wanafunzi wasio na vikalio kutoka wanafunzi 188,060 na kufikia 162,678 sawa na asilimia 13.5%. Kwa hivyo, jumla ya vikalio vinavyohitajika kwa sasa ni madawati 41,122, Viti 42,204 na Meza 42,824.

Mhe. Spika, ningependa kutoa wito kwa wananchi wa Zanzibar na walio nje ya Zanzibar kuzidi kujitolea katika kufanikisha kampeni za kuchangia vikalio maskulini. Kama sote tunavyoelewa vikalio vinaimarisha na kushajihisha mazingira ya kufundisha na kujifunzia. Pia vikalio vinapunguza utoro mashuleni na kuimarisha afya za walimu na wanafunzi wakati wa kufundisha. (*Makofi*)

Mhe. Spika, suala la kulipa Kodi ni suala muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Kama tujuavyo Serikali zote duniani zinaendeshwa na makusanyo yanayotokana na kodi. Napenda kuchukuwa fursa hii kuwapongeza wafanyakazi wote wa *ZRB* kwa kazi zao nzuri za ukusanyaji wa kodi. Aidha nawapongeza kwa kuanzisha

operesheni mbali mbali ambazo lengo lake ni kuhakikisha kila mwananchi analipa kodi ipasavyo. Wito wangu kwa wananchi wote wa Zanzibar tulipe kodi, tena kwa wakati. Tusipofanya hivyo tunaitia nchi yetu umaskini, kodi ipo kwa ajili ya maendeleo yetu wenyewe. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mvua za vuli zimeshaanza kunyesha nchini. Ni wajibu wetu Waheshimiwa Wawakilishi kuwahimiza wananchi wetu kuzitumia vizuri mvua hizi, kwa kupanda mazao ya kudumu ambayo ni pamoja na mazao ya chakula na ya biashara.

Aidha, naomba tuendelee kufuata maelekezo yote ya wataalamu wa afya, yanayotutaka kujikinga na maradhi ya kuambukiza ikiwemo matumbo ya kuharisha na kipindupindu. Mwaka huu jumla ya wagonjwa 342 waliugua kipindupindu, baada ya kipindi cha mvua kama ilivyo kawaida yetu kutokana na kutobadilika tabia zetu, hasa kutupa taka ovyo, kutupa *pampas* katika michirizi ya maji ya mvua ambayo huchafua njia za maji safi hasa pale panapotokea mafuriko. Idadi hii ni ndogo ukilinganisha na idadi ya mwaka jana wagonjwa 652, waliugua kipindupindu na vifo kadhaa vilitokezea. Hii inaonyesha dhahiri kuwa inawezekana kutokomeza kipindupindu Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri, Mwenyezi Mungu ametunusuru mwaka huu hakuna kifo kilichotokea kutokana na maradhi haya ya mripuko wa kipindupindu. Wito wangu kwa Wawakilishi wote wa wananchi, viongozi na wananchi wenyewe hasa wanaokaa katika maeneo hatarishi yanayojulikana kwa athari za kipindupindu na matumbo ya kuharisha, kuchukua tahadhari kubwa zaidi na kuwa wasimamizi sisi wenyewe wa kukataza uchafuzi wa mazingira, kutupa taka ovyo, kuhakikisha vyanzo vya maji iwe kisima au maji ya chemchem yapo mbali na mashimo ya vyoo.

Mhe. Spika, utumiaji wa maji safi yaliyochemshwa ni muhimu sana, pamoja na vidonge vya *chlorine*, kuhakikisha chembechembe za vinyesi vyenye vimelea vya kipindupindu vinatoweka. Serikali tayari imeshaweka mpango maalum wa kutokomeza kipindupindu ambao unajumuisha sekta kadhaa ikiwemo sekta ya afya, sekta ya maji kupitia *ZAWA*, Tawala za Mikoa na Halmashauri na Manispaa za Wilaya kwa ajili ya usafi wa maeneo yetu na michirizi, pamoja na karo za maji machafu, zote hizo zikisimamiwa na Idara ya Maafa kwa ajili ya kinga ya maradhi haya thakili. Zanzibar bila ya kipindupindu inawezekana sote tukiunganisha nguvu zetu kwa pamoja tunaweza kutokomeza kipindupindu Zanzibar. Kama bado wapo watu wanaoishi mabondeni, ni vyema wahame kutoka maeneo hayo ili kunusuru maisha yao na mali zao.

Mhe. Spika**,** Serikali yetu ya Mapinduzi ni serikali sikivu kwa sababu ni serikali ya wananchi. Nawasihi wajumbe wenzangu tunapochangia au kuikosoa serikali ni vyema tukatumia lugha inayoendana na utamaduni na silka zetu. Tusipokuwa waangalifu wa matumizi ya maneno Baraza letu tukufu litapoteza heshima machoni mwa wananchi wetu. Maneno makali ya kashfa au kejeli tukubaliane iwe sasa basi, ili Baraza letu liendelee kuwa chemchem ya maneno ya stara na busara. Nasaha zangu hizi hazina maana ya kuwafumba midomo isipokuwa ni wajibu wetu sote kutumia lugha inayokubalika Barazani hapa. Lugha za kejeli dhidi ya serikali au chama tawala haziwezi kuleta tija yoyote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baadhi ya wanasiasa wetu nchini wamekumbwa na maradhi sugu ya kuota mchana; na maajabu ya ndoto zao hizo huwa zinahusu kitu kimoja tu nacho ni kukalia kiti cha Urais wa Zanzibar. Wataalamu wa ndoto wanasema ndoto za mchana huwa ni uongo. Nakubaliana na wataalamu hawa kwani kiti cha urais wa Zanzibar ni kimoja na tayari kimeshakaliwa na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, ambaye amechaguliwa na wananchi kwa kufuata taratibu zote za kidemokrasia, na hakitakuwa wazi mpaka miaka mitano imalizike, yaani mpaka 2020. Sasa mwenye ndoto hizo asubiri hadi hapo mwaka 2020 ajaribu bahati yake ingawa wengine wameshajaribu sana bila mafanikio. Ni vyema sasa akamuachia mwenzake naye ajaribu. *(Makofi)*

Nasaha zangu kwa wananchi wenzangu, kuachana nao wanasiasa wanaoota mchana kwani watawapotezea muda wenu bure wa kushughulikia maisha yenu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wakati wa kujadili ripoti ya Mamlaka ya Maji (*ZAWA*), Waheshimiwa Wajumbe katika michango yao walionyesha hisia kali zao kuhusu kutopatikana kwa maji katika maeneo yao. Serikali imewasikia, na kama mnavyosema wenyewe, serikali yenu hii ni serikali sikivu kwa sababu ipo kwa ajili ya kuwatumikia wananchi. Mimi nayaunga mkono maelezo ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Serikali itakapopokea mahitaji halisi na gharama zote ambazo *ZAWA* inataka ili maji yaweze kupatikana katika maeneo yanayolalamikiwa na mengine. Hivyo, naiomba Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji, kuleta serikalini haraka iwezekanavyo mahitaji halisi yanayohitajika na Mamlaka ya Maji, ili serikali iweze kuzitafuta fedha hizo. Tusingependa kupata makisio ya kijumla kwa kufanya hivyo kutakuwa ni kucheleweshe mambo maana serikali haitayakubali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mwisho napenda kukushukuru tena wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza, kwa kutuongozea Baraza lako hili tukufu kwa heshima, busara na umakini mkubwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kumalizia niwatakieni Waheshimiwa Wawakilishi kila la kheri, na mafanikio katika kuwatumikia wananchi wenu majimboni mwenu. Nawaomba sana mrudi majimboni mwenu mkawasaidie wananchi wenu kutatua kero zao zinazowakabili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumatano tarehe 06 Disemba, 2017 saa 3.00 barabara za asubuhi panapo majaaliwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, sasa naomba niwahoji wale wote ambao wanaunga mkono hoja ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwamba tuahirishe mpaka tarehe 06/12/2017 wanyanyuwe mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

Waheshimiwa Wajumbe, napenda kuchukua nafasi hii na mimi kutoa shukrani zangu za dhati sana, kwanza kabisa kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa hotuba ambayo sio ndefu fupi sana, lakini nakubaliana na nyinyi kwamba ilikuwa nzito sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nimepungukiwa na maneno. Haikuwa na maneno mengi sana lakini maudhui yamekuwa mazito sana. Ushahidi ni hiyo furaha ambayo mmeionesha baada ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kumalizia kusoma hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha naomba nitowe tangazo. Nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe, wale wote ambao wanakwenda kwenye kilele cha Sherehe za Mwenge, wanaarifiwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 14/10/2010 gari zitaondoka Baraza la Wawakilishi kongwe saa 1:00. Kwa wale waendaji wote watatakiwa wawepo pale.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hapo sasa napenda sasa kuahirisha shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka siku ya Jumatano tarehe 06/12/2017, saa 3:00 barabara za asubuhi panapo majaaliwa. Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba mnyanyuke ili tupate wimbo wa taifa. Wimbo wa Taifa.

(WIMBO WA TAIFA)

(Saa 11:30 jioni Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 06 Disemba, 2017 saa 3:00 za asubuhi)